



LOWELL PUBLIC SCHOOLS

DEPARTMENT OF SPECIAL EDUCATION

(IDARA YA ELIMU MAALUM)

Henry J. Mroz Administration Office
155 Merrimack Street, 5th Floor
Lowell, Massachusetts 01852

Michael Lovato, Mkurugenzi wa Elimu Maalum

Donna Maluccio & Ashley Pennell, Wakurugenzi Wasaidizi wa Elimu Maalum

Simu: (978) 674-4322

Faksi: (978) 275-6361

4/24/20

Kwa familia zetu za Lowell tunazothamini,

Tunatarajia ya kwamba mtapokea ujumbe huu ilihali nyinyi na familia zenu mko salama na wenye afya. Tunaelewa kikamilifu namna kufungwa shule kwa lazima kwa sababu za afya ya umma zimeathiri familia zote na kila mtu kwa jamii yetu. Tunafahamu namna athari hii ni ngumu zaidi kwa familia za wanafunzi wenye ulemavu. Tunashukuru ufahamu wenu, ushirikiano wenu na usaidizi wenu tunapopitia wakati huu mgumu kama jamii ya shule. Ujumbe huu unatolewa ili kuarifu namna huduma na mwendo wa elimu maalum utafanyika katika muda huu wa kufunga shule kwa lazima.

Tukiambatana na miongozo kutoka serikali shirikisho na ya eneo, tutasogelea awamu inayofuata ya mafunzo ya mbali – kutoa fursa zilizoelekezwa za mafunzo ya mbali. Katika awamu hii, Huduma za elimu zitatolewa kwa namna tofauti na namna angepewa mtoto wako iwapo angekuwa katika darasa la kikawaida katika mpango wake wa shule. Wafanyikazi wa Elimu Maalum wa Shule ya Lowell Public Schools watarejelea mahitaji ya mtoto wako kulingana na IEP ya sasa ili kuamua mbinu zenye ubunifu zinazoweza utoaji wa huduma za kielimu na huduma zinazohusika katika jukwaa la mafunzo ya mbali. Tunakiri ya kwamba hili ni changamoto tofauti kwa Jamii ya shule ya Lowell Public School kwa hivyo tunapanga kushughulikia na kusuluhisha changamoto hili pamoja.

Vitu kadhaa za kukumbuka tunapoanzisha huduma za mafunzo ya mbali:

1. Hii ni jambo mpya kabisa. Hatumo katika jengo la kawaida ilihali tunatakiwa kuwapatia wanafunzi wetu mazoezi ya kielimu. Itakuwa jukumu letu kuhakikisha wanafunzi wetu wana fursa ya kulinda uhusiano na walimu wao, wanafunzi wenzao, na waliojifunza katika mwaka. Ili kufanikiwa, huduma hizi zitaonekana kuwa tofauti na yale yaliyoorodheshwa katika IEP ya sasa.
2. Jukumu za elimu maalum za serikali shirikisho na serikali ya eneo hazijaondolewa; tuatakiwa kufanya tuliyokuwa tunafanya awali – tunayofanya sasa – kukidhi mahitaji ya wanafunzi wetu. Jukumu za serikali shirikisho hazijabadilika na si mpya.
3. Tunafaa kukumbanisha jukwaa hili mpya pamoja na tunayoyajuwa sasa kuhusu wanafunzi wetu na mahitaji yao ili kufanya mpango wa kufaa zaidi wa mafunzo ya mbali tunayoweza. Hatuwezi kuiga nidhamu ya utoaji huduma ambapo mafunzo yanatendeka ndani ya shule LAKINI tunaweza kuamua Vigezo & Rasilimali na Maagizo & Huduma zinazofaa kwa kila moja wa mwanafunzi wetu.

Yanayofuata ni miongozo ya kuzingatia unapofikiria kila mwanafunzi kibinafsi na nini atahitaji katika muda huu shule zikiwa zimefungwa. Maoni yanatolewa tukiwa na vigezo viwili kwa akili: kiwango cha hitaji cha kila mwanafunzi na eneo mbili ambazo DESE inatuhitaji tuzingatia katika utoaji wa fursa za kielimu kwa wanafunzi: 1) Vigezo & Rasilimali, na 2) Maagizo & Huduma. Kwa ziada, tafadhali kumbuka kwamba tunafaa kuweka umuhimu katika kipengele cha “ubinafsi” katika Programu ya Elimu ya Kibinafsi (IEP). Hili linamaanisha kwamba, kulingana na elimu yako ya kitaalam na ufahamu wako wa wanafunzi wako, unaweza kuamua kuongeza au kupunguza viwango zilizopendekezwa – hii ni sawa, ili mradi mahitaji ya kibinafsi ya wanafunzi wako yanatimizwa kwa mbali.

Timu za Elimu Maalum zitawasiliana na wewe ili kutengeneza mipango ya mafunzo ya mbali ya muda zinazopatia kila mwanafunzi rasilimali na vigezo wanazohitaji ili kutegemeza jukwaa la mafunzo ya mbali. Mpango wa mafunzo ya mbali ya muda haitabadilisha huduma zako zilizo katika IEP yako ya sasa na itashughulikia huduma katika muda wa kufungwa shule pekee. Mipango ya mafunzo ya mbali ya muda yatashughulikia huduma za elimu na huduma zinazohusiana katika jukwa la mbali na itakaa tofauti na inapoonekana katika mpango wa sasa.

Unapotengeneza mpango wa Mafunzo ya Mbali ya Muda tafadhali elewa kwamba hatutahitaji kupata rhusa ya mzazi lakini wilaya inatakiwa kutoa ilani. Wilaya pia inaamini kwamba ni muhimu kuwasiliana na wazazi na kuongeza habari yote muhimu na inayofaa kwa mafanikio ya mwanafunzi wako katika muda huu.

Taratibu zinazofuata zitafanyika iwapo:

1. **Muda wa mapitio ya mwaka au tathmini ya mwanafunzi wako umefika** – timu ya elimu maalum itafanya mkutano kupitia jukwaa za mafunzo ya mbali zinazoweza kupatikana kwa wahusika wote. Iwapo wewe kama mzazi au mlezi utachagua kutofanya mkutano wa IEP katika muda huu wa kufungwa shule wa muda, uamuzi wako utaheshimiwa na timu litafanya mkutano baada ya shule kufunguliwa.
2. **Mwanafunzi wako alikuwa katika hali ya tathmini ya awali lakini hakutathminiwa** – timu ya elimu maalum itaendelea na tathmini shule ikifunguliwa tena.
3. **Tathmini ya mtoto wako haikukamilishwa** – timu ya elimu maalum itafanya mkutano katika jukwaa ya mafunzo ya mbali na kukamilisha mkutano wa kuamua tathmini. Iwapo mwanafunzi wako atastahiki huduma basi mpango wa mafunzo ya mbali ya muda utatengenezwa kupitia mpango wa mafunzo ya mbali. Shule itakapofunguliwa timu itafanya mkutano tena ili kutengeneza IEP.
4. **Mtoto wako anaendelea kutoka programu ta miaka 3 na anastahiki huduma za elimu maalum** – utahitaji kumsajili mtoto wako katika na shule ya Lowell public schools na utapatiwa mpango wa mafunzo ya mbali ya muda.
5. Maombi yoyote ya tathmini ya awali au tathmini zaidi yatakamilishwa shule zitakapofunguliwa tena.

Tungependa kukutakia mema katika muda huu wa mgogoro wa kibinafsi na kijamii. Tunaendelea kujitolea katika mafanikio ya mtoto wako na tunajitolea kufanya kazi kwa bidii kujitoka kutoka janga hili. Utoaji wa huduma za elimu maalum unaendelea kuwa kipaumbele wetu wa juu zaidi, na tunatarajia ushirikiano wa kuendelea katika kukidhi mahitaji ya mwanafunzi wako.

Michael Lovato, Mkurugenzi wa Elimu Maalum